**Taarifa kwa vyombo vya habari vya Global Witness**
**Chini ya vikwazo hadi 00:01 saa za Uingereza siku ya jumatatu tarehe 4 desemba 2023**

## Kampuni kubwa ya Ufaransa ya TotalEnergies imehusishwa kwa kutishia jamii zilizoathiriwa na bomba la mafuta lenye utata.

- *Uchunguzi mpya wa Global Witness unafichua ushahidi kwamba TotalEnergies imehusishwa na vitisho kwa jamii zilizoathiriwa na mradi tata wa EACOP nchini Uganda na Tanzania, huku wanajamii wakiripotiwa kushinikizwa kutia sahihi mikataba ya fidia ya ardhi yao.*
- *Katika matukios kadhaa, uchunguzi ulipata ushahidi unaopendekeza kuwa TotalEnergies iliwasiliana na mamlaka ya serikali ya Uganda kabla kutolewa kwa vitisho na kutiwa kizuizini kwa wanaharakati wanaopinga uchimbwaji wa mafuta.*
- *TotalEnergies pia inashtumiwa kwa kudharau unyanyasaji na watetezi wa 'kuwasha gesi'*
- *Global Witness sasa inatowa mwito kwa uchunguzi huru kufanywa ili kubaini jukumu la TotalEnergies katika ukandamizaji huu dhidi ya watetezi wa ardhi na mazingira.*

Jukumu la kampuni kubwa ya mafuta ya Ufaransa ya TotalEnergies katika kutisha na kulipiza kisasi dhidi ya jamii zilizoathiriwa na mradi wa mafuta ya kisukuku wa dola bilioni 5 nchini Uganda na Tanzania limetiliwa shaka katika uchunguzi mpya [WEKA KIUNGO] iliyofanywa na Global Witness.

Kwa kuungwa mkono na TotalEnergies na makampuni ya mafuta ya serikali, Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) tayari limesababisha usumbufu mkubwa kwa wale wanaoishi kando ya njia inayopendekezwa kuwekwa bomba la kilomita 1,440. Mradi huo unatarajiwa kuwa na athari mbaya kwa mazingira, na makadirio ya uzalishaji wa karibu tani milioni 380 za gesi ya CO2 katika muda wake wa maisha wa miaka 25 - zaidi ya yale ya taifa la Uingereza katika mwaka wa 2022.

Uchunguzi uliochapishwa leo ulikuta kuwa TotalEnergies na wanakandarasi wake wamekuwa wakitoa vitisho kwa jamii zilizoathiriwa na EACOP - hata pale uchunguzi ulipofanywa na mamlaka za serikali. Madai mengi yamenakiliwa na wanajamii waliohisi kushinikizwa kukubali mikataba ya fidia ya ardhi yao chini ya thamani yake halisi, huku baadhi ya jamii zikiripoti kulazimishwa kutia sahihi mikataba papo hapo. Wengine waliripoti kutopewa muda wa kutosha kuelewa hati walizokuwa wakitia sahihi.

Bali ya matokeo haya, uchunguzi unafichua ushahidi kwamba vitisho na kuzuiliwa kwa wanakampeni kadhaa uliofanywa na mamlaka za serikali ulifanyika *baada ya* kupingwa kwa ujenzi wa bomba hilo. Katika visa kadhaa, mamlaka za serikali zilionekana kuwawasiliana na TotalEnergies kabla ya tukio za kulipiza kisasi.

Tangu Septemba 2020, takriban wanaharakati 40 nchini Uganda pekee wamezuiliwa kwa kuzungumza dhidi ya mafuta au bomba, huku wengine wakidai kuwa wamepigwa wakiwa kizuizini.

Ripoti hiyo inaangazia kwamba iwapo TotalEnergies itapatikana kulingana na uchunguzi zaidi kuwa ilitoa taarifa ikijua kuwa kisasi dhidi ya watetezi kinaweza kufuata, hii inaweza kuishurutisha kuwajibika kwa  kampuni hiyo ambayo inamiliki karibu theluthi mbili ya EACOP.

**Hanna Hindstrom, Mpelelezi Mwandamizi wa Kampeni ya Watetezi wa Ardhi na Mazingira katika Global Witness alisema:** *"Kulipiza kisasi dhidi ya wanaharakati katika mataifa haya yaliyo na utawala wa  kimabavu kumesababisha athari mbaya kwa jamii zilizoathiriwa na bomba hilo na asasi za kiraia nchini Tanzania na Uganda, huku wengi wakiripotiwa kuogopa kuongea bila uoga. Kama wamiliki hisa wakuu katika EACOP, ni muhimu kwamba kushiriki kwa njia yoyote kwa TotalEnergies ' katika kukamatwa , mashambulizi na kulipiza kisasi  dhidi ya  wale walioathiriwa na mradi uchunguzwe zaidi."*

Uchunguzi pia ulipata ripoti kwamba wakandarasi wa TotalEnergie waliwatishia watetezi wanaopigania fidia. Mlinzi mmoja mashuhuri, ambaye kauli yake inaungwa mkono na shahidi, anasema mwanakandarasi alimtishia kukamatwa kwa "kuhujumu programu za serikali " kama asingelikubali fidia yake. Katika tokeo lingine, mkandarasi anaonekana kumtisha mkulima kule Uganda aliyejipata katika mzozo na kampuni hiyo kwa kujenga uzio kuzunguka nyumba yake - ingawa TotalEnergies inakanusha hili na kusisitiza kuwa uzio huo uliwekwa kwa ridhaa yake na kwa "usalama" wake. Baadhi  wale wanaohusika katika mizozo wanasema wamelazimika kujificha.

Uchunguzi huo unaangazia jinsi  uchache wa taarifa kuhusu ulipizaji kisasi na kukamatwa kwa wanaharakati nchini Tanzania kutokana na kukosekana kwa nafasi kupigania uraia nchini humo, huku ripoti ikibainisha kuwa kwa sasa kuna "marufuku" madhubuti kwa harakati zozote zinazoonekana kuwa 'kupinga serikali'. , iliyotumika kuwanyamazisha wanakampeni.

Inabainisha kuwa wanaharakati wawili wa Tanzania walilazimika kutoroka nchini mapema mwaka huu kwa ajili ya kuandaa mkutano na waandishi wa habari wakielezea wasiwasi wao kuhusu EACOP, baada kupikea vitisho. Waliporudi nyumbani, walikutana na polisi, nyumba zao zikapekuliwa na pia wakapokonywa  simu na taklishi.

Mwanaharakati mwingine wa Tanzania Baraka Machumu alitoroka nchini mwaka 2022 akihofia usalama wake. Aliripoti kufuatwa na kunyanyaswa nyumbani kwake kufuatia ziara yake katika makao makuu ya TotalEnergies akiwa na wanahabari wawili, ambapo alihojiwa na afisa wa usalama wa TotalEnergies . Hakuna ushahidi wa moja kwa moja kwamba Machumu alitishiwa na wafanyikazi wa TotalEnergies au kwa maagizo yao.

**Baraka Machumu, Mwanzilishi wa Green Conservators nchini Tanzania, alisema** : " *Ukipinga kipengele chochote cha bomba la mafuta nchini Tanzania, utalengwa. Imenilazimu kufunga ofisi yangu na hata kuitoroka  nchi ili kuepuka kulipizwa kisasi kwa kazi yangu.*

*"Hatuwezi kusaidia jamii ambazo zitapoteza ardhi na maisha kwa bomba bila  sisi na hao kukabiliwa na  hatari ya kuzuiliwa na kukamatwa. Tunahitaji mjadala kuhusu mustakabali wa EACOP, sio kunyamazishwa kwa  wale walioathirika zaidi kutokana na ujenzi wake."*

Global Witness pia iliarifiwa kuhusu kulipiza kisasi dhidi ya watetezi wanaoshukiwa kuhusika katika malalamiko ya kisheria. Baada ya kutuma barua kwa EACOP na Total, jamii ziliripoti kupokea simu kutoka kwa maafisa wa serikali za mitaa wakiwauliza kuhusu jukumu lao katika hatua ya kisheria, na kuuliza ni nani wanaoshirikiana nao.

Ripoti hiyo inadai kuwa TotalEnergies inafaidika kutokana na nafasi ya kimabavu ya kisiasa nchini Tanzania, na kukandamizwa pakubwa kwa juhudi za uhamasishaji wa mashirika ya kiraia karibu na bomba hilo.

Uchunguzi huo pia unaangazia swala la juhudi zaa kampuni hiyo kutaka kuhakikisha kuwa Tanzania inachaguliwa kuwa mkondo wa bomba hilo badala ya nchi jirani ya Kenya, ambako ujenzi ulipangwa awali. Inabainisha kuwa ardhi nchini Tanzania inamilikiwa na rais wa nchi hiyo - na kuifanya iwe rahisi kwa Kampuni ya EACOP kupata ardhi.

Vitendo hivi vinavyodaiwa kuhusisha TotalEnergies na wakandarasi wake vilivyoandikwa katika uchunguzi vinaweza kujumuisha ukiukaji wa viwango vya kimataifa vya utwaaji ardhi pamoja na Kanuni za Umoja wa Mataifa.

Lakini katika kujibu ombi la Global Witness la kutoa maoni, TotalEnergies ilikanusha ‘’kwa dhati’’ kwamba kampuni tanzu ya Total Energies EP Uganda (TEPU) na EACOP Ltd ziliwatisha wanajamii kusaini makubaliano yoyote ya fidia. Ilisisitiza kwamba walizingatia viwango vya kimataifa vya fidia na kutoa fidia kwa "gharama kamili ya uhamishwaji", pamoja na "malipo ya kuinua maisha" na kutoa msaada mwingine kwa wale waliohama. Pia iliongeza kusema  kuwa jamii zilipewa mawakili na pia huduma za utafsiri kwa mujibu wa sheria, na kwamba karibu 95% ya walioathirika walikubali fidia hiyo.

TotalEnergies pia ilikanusha vikali kwamba walipuuza majukumu yao ya biashara na haki za binadamu au kwamba walifanya chochote ili kusababisha  hali ya hofu. Wanasema kuwa EACOP Ltd na TEPU haziruhusu vitisho au vitisho vyovyote kwa wale walioathiriwa na bomba hilo, na kuwa huchunguza madai hayo.

Kujibu madai kwamba imeshiriki katika  unyanyasaji wa serikali, TotalEnergies ilidai kuwa "haiwezi kuwajibika" kwa vitendo vya wahusika wasiohusiana nao na kukana uhusiano wowote na " tabia isiyo halali ".

TotalEnergies na timu ya EACOP pia walipuuza madai ya kulipiza kisasi dhidi ya mashirika ya kiraia yanayofanya kazi ya kuchimba mafuta nchini Uganda katika mkutano na Global Witness mapema mwaka huu, wakidai kwamba: "Kila mara tunaposikia madai ya ukiukaji wa haki za binadamu, tunachunguza... Lakini hakuna ushahidi kwamba madai hayo ni sahihi.”

**Maxwell Atuhura, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti ya Tasha nchini Uganda, alisema:** *"Kama mtetezi wa mazingira dhidi ya kuchimbwa kwa mafuta nchini Uganda, nimehukumiwa , nimenyanyaswa na nimekamatwa.*

*"Kwa kupuuza mashambulio dhidi ya uhuru wa kujieleza nchini Uganda, TotalEnergies inadhoofisha na kuwadunisha watetezi wanaoishi kwa hofu. Hii ni aibu. Kampuni zote mbili za mafuta na serikali ya Uganda zinahitaji kuwajibika."*

/

**MWISHO**

Tangazo la uwajibikaji :Toleo la Kiswahili ni tafsiri ya hati asili kwa lugha ya kiingereza. Iwapo kutakuwa na tofauti yoyote kati ya chapisho kwa lugha ya Kiswahili na lile la kiingereza, toleo la kiingereza ndilo litakuwa toleo rasmi na lenye mamlaka.

**Vidokezo kwa Wahariri**

Uchunguzi huu utachapishwa **tarehe 4 desemba 2023 00:01 GMT** na uko chini ya vikwazo vikali hadi wakati huu.

Ripoti hiyo itapatikana katika tovuti ya www.globalwitness.org

**Anwani**

Evie Calder, Mshauri Mkuu wa Mawasiliano, Kampeni ya Watetezi wa Ardhi na Mazingira, Shahidi wa Kimataifa Global Witness
E: ecalder@globalwitness.org | M: +447872 600870